TOLEO MAALUMU Na. 020 | AGOSTI 2026 | HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM

Jarida la

SAUTI YA JIJI

TOLEO MAALUMU



HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM YAIBUKA MSHINDI WA KWANZA NANENANE KANDA YA MASHARIKI 2026

"Tambua Soko; Ongeza Tija Kutekeleza Dira 2050"



HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM YAIBUKA MSHINDI WA KWANZA 88 KANDA YA MASHARIKI 2026

Na Mwandishi wetu – Halmashauri ya Jiji la DSM

Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imeibuka Mshindi wa Kwanza kwa Mkoa wa Dar es Salaam na Mshindi wa Kwanza wa Jumla katika Maonesho ya Nanenane Kanda ya Mashariki 2026, ushindi unaodhihirisha ubunifu, matumizi ya teknolojia na jitihada za Jiji katika kukuza kilimo chenye tija.

Tuzo hizo zimetolewa Agosti 8, 2026 na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Watu Wenye Ulemavu), Prof. Palamagamba John Kabudi, aliyekuwa Mgeni Rasmi katika kilele cha maonesho hayo yaliyofanyika Viwanja vya Nanenane, Morogoro.

Ushindi huo umechangiwa na namna Halmashauri ilivyowasilisha fursa, ubunifu na teknolojia mbalimbali katika kilimo, pamoja na elimu iliyotolewa kwa wananchi kuhusu fursa za kilimo cha kisasa na

cha mijini.

Akizungumzia umuhimu wa kuendeleza elimu hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Mhe. Edward Mpogolo, amesema:

“Tuendelee kuwajengea uwezo wakulima juu ya namna bora ya kufanya kilimo chenye tija, ili waweze kuongeza uzalishaji, kupata masoko na hatimaye kuboresha maisha yao.”

Kwa upande wake, Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Nurdin Bilal ‘Shetta’, amesema Jiji litaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ushiriki katika maonesho ya Kanda ya Mashariki.


“Tutaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ushiriki wa maonesho haya ya Kanda ya Mashariki. Maonesho haya yanaonesha kuwa hata wakazi wa maeneo ya mjini wana fursa za kufanya kilimo mjini chenye tija,” amesema Mstahiki Meya Nurdin Bilal ‘Shetta’.

Naye Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Elihuruma Mabelya, amesema teknolojia inatoa fursa ya kuifanya sekta ya kilimo kuwa sehemu muhimu ya uchumi wa jiji.

“Tunapaswa kuangalia kilimo kama sehemu ya uchumi wa jiji. Teknolojia inatoa fursa ya kufanya kilimo mjini kwa ufanisi zaidi, kuongeza uzalishaji na kipato,” amesema Mabelya.

Ushindi huo unaendana

BANDA LA HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM, MOROGORO.



na kaulimbiu ya Nanenane 2026, “Tambua Soko; Ongeza Tija Kutekeleza Dira 2050,” na unaonesha namna Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ina-vyotumia maarifa, teknolojia na ubunifu kukuza kilimo cha mijini na kufungua fursa za chakula, ajira na kipato.







DARASA LA KILIMO CHA KISASA LINAVYOFUNGUA FURSA KATIKA JIJI LA DAR ES SALAAM





Na Mwandishi wetu – Halmashauri ya Jiji la DSM

Katika jiji linalokua kwa kasi kama Dar es Salaam, kilimo kinaendelea kuwa sehemu muhimu ya maisha ya wananchi. Mbali na kuwa chanzo cha chakula, kilimo ni fursa ya ajira, kipato na shughuli za kiuchumi kwa familia na jamii.

Ingawa mazingira ya mijini yana changamoto ya upatikanaji wa maeneo makubwa ya kilimo, maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu yamefungua njia mpya za kufanya kilimo katika maeneo madogo na kutumia rasilimali zilizopo kwa ufanisi.

Kituo cha Rasilimali Kilimo – Pugu Kinyamwezi, kilichopo chini ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, ni daraja kati ya wananchi na maarifa ya kilimo cha kisasa.

Kituo hiki kinawapa wananchi fursa ya kujifunza kwa vitendo mbinu mbalimbali za uzalishaji, matumizi ya teknolojia na namna ya kuongeza tija katika kilimo, ikiwemo katika mazingira ya mijini.

WIKI YA ELIMU, TEKNOLOJIA NA FURSA ZA KILIMO

Katika kuadhimisha Siku ya Wakulima na Wafugaji, Nanenane, kuanzia tarehe 1 hadi 8 Agosti 2026, Kituo cha Rasilimali Kilimo Pugu Kinyamwezi kilitumika kuwafikishia wananchi elimu ya kilimo bila malipo.

Kupitia kituo hicho, wananchi wanapata fursa ya kujifunza kuhusu uzalishaji wa mazao, afya ya udongo, umwagiliaji, uvunaji wa maji ya mvua, matumizi ya matandazo, usindikaji wa mazao pamoja na matumizi ya teknolojia za kisasa katika kilimo.

Elimu hii inazingatia uhalisia wa mkulima wa sasa ambaye si lazima awe na eneo kubwa la ardhi ili kuzalisha. Kinachohitajika ni maarifa sahihi ya kutumia eneo na rasilimali zilizopo kwa ufanisi.

Hatua hii inaendana na kaulimbiu ya Nanenane ya mwaka huu isemayo “Tambua Soko; Ongeza Tija Kutekeleza Dira 2050”, inayolenga kuongeza tija, thamani ya mazao na ushindani katika masoko ya ndani na kimataifa.

SHAMBA DARASA

Pugu Kinyamwezi si kituo cha nadharia pekee, bali ni eneo ambalo wananchi wanaweza kuona, kujifunza na kuelewa kwa vitendo namna kilimo cha kisasa kinavyotekelezwa.

Katika kituo hicho, wananchi wanaweza kujifunza mbinu za uzalishaji wa mazao mbalimbali ikiwemo nyanya, migomba, mahindi, pasheni, papai, uyoga, tembele, nyanya chungu na biringanya.

Uwepo wa mazao hayo unatoa fursa kwa wananchi kuona namna mazao yanavyoweza kuzalishwa, kutunzwa na kusimamiwa kwa kutumia mbinu bora za kilimo.

Kwa mkazi wa jiji mwenye eneo dogo, ujumbe unaotoka Pugu Kinyamwezi ni kwamba ukubwa wa eneo sio kikwazo cha uzalishaji. Kwa maarifa na teknolojia sahihi, hata eneo dogo linaweza kuwa chanzo cha chakula na kipato.

AFYA YA UDONGO

Kabla ya mkulima kuanza kuzalisha, ni muhimu kufahamu hali ya udongo anaotumia. Ndiyo maana upimaji na elimu kuhusu afya ya



udongo ni sehemu muhimu ya mafunzo yanayotolewa Pugu Kinyamwezi.

Taarifa kuhusu hali ya udongo humsaidia mkulima kuelewa mahitaji ya eneo lake na kufanya maamuzi sahihi kuhusu matumizi ya mbolea na virutubisho vinavyohitajika na zao husika.

UMWAGILIAJI WA KISASA WAFUNGUA FURSA PUGU KINYAMWEZI

Maji ni rasilimali muhimu katika kilimo, na matumizi yake kwa ufanisi ni sehemu ya kilimo cha kisasa.

Kwa kufanya hivyo, matumizi ya pembejeo yanaweza kuwa na ufanisi zaidi, huku mkulima akipunguza matumizi yasiyo ya lazima na kuongeza uwezekano wa kupata mavuno bora.

Hapa ndipo sayansi na teknolojia vinapounganishwa na uzoefu wa mkulima, na kuifanya kilimo kuwa shughuli inayotegemea taarifa sahihi badala ya mazoea pekee.

Kituo cha Pugu Kinyamwezi kinatoa elimu kuhusu umwagiliaji wa mfumo wa matone, unaosaidia kupeleka maji karibu na eneo la mmea kwa kiwango kinachohitajika.

Wananchi pia wanajifunza matumizi ya matandazo ya plastiki, yanayoweza kusaidia katika kuhifadhi unyevu na kudhibiti magugu, pamoja na uvunaji wa maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya umwagiliaji.

Mbinu hizi zina umuhimu mkubwa katika kilimo cha mijini kwa kuwa zinasaidia mkulima kutumia rasilimali chache kwa ufanisi na kuendeleza uzalishaji katika mazingira yenye changamoto ya upatikanaji wa maji.



TEKNOLOJIA YA DRONE YABADILI KILIMO, YAONGEZA UFANISI SHAMBANI

Kadiri teknolojia inavyoendelea kuingia katika sekta ya kilimo, shughuli za shambani nazo zinabadilika.

Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam inaonesha matumizi ya drone za kilimo, zikiwemo



zinazoweza kusaidia katika shughuli za shambani kama usambazaji wa maji au pembejeo, kutegemea aina ya drone na vifaa vinavyotumika.

Teknolojia hii inasaidia kupunguza muda na nguvu kazi katika baadhi ya shughuli za uzalishaji, kuongeza usahihi na kurahisisha usimamizi wa shughuli za shamba.

Uwepo wa teknolojia hiyo katika mafunzo ya kilimo unaonesha mwelekeo mpya wa sekta hii: kilimo cha kisasa hakiwezi kutenganishwa na sayansi, teknolojia na ubunifu.

KUTOKA SHAMBANI HADI SOKONI

Kuongeza uzalishaji ni hatua muhimu, lakini si mwisho wa safari ya mkulima. Thamani ya zao inaweza kuongezeka zaidi kupitia usindikaji, uhifadhi na ufungashaji unaokidhi viwango vya soko.

Kwa kutambua hilo, Kituo cha Rasilimali Kilimo Pugu Kinyamwezi kinatoa pia elimu kuhusu njia sahihi za usindikaji wa mazao ya kilimo.

Usindikaji husaidia kuongeza thamani ya mazao, kupunguza upotevu baada ya mavuno na kufungua fursa za masoko mapana zaidi.

Hii inaendana na ujumbe wa Nanenane wa “Tambua Soko; Ongeza Tija”. Mkulima anahitaji kufahamu anachozalisha, nani atakinunua na namna ya kuongeza thamani ya bidhaa yake ili kupata faida zaidi.

KILIMO CHA MIJINI: ARDHI NDOGO, FURSA KUBWA

Kwa jiji kama Dar es Salaam, kilimo cha mijini kina nafasi muhimu katika kuongeza upatikanaji wa chakula, ajira na kipato.

Pugu Kinyamwezi kinaone-

sha kwa vitendo kwamba kilimo kinaweza kuendelezwa katika mazingira ya mijini kwa kutumia mbinu zinazofaa, zikiwemo umwagiliaji wa matone, uvunaji wa maji ya mvua, matandazo, uzalishaji wa uyoga na teknolojia nyingine.

Hivyo, kilimo cha mijini hakipaswi kuonekana kama shughuli ndogo isiyo na thamani. Kwa matumizi sahihi ya teknolojia, maarifa na ubunifu, eneo dogo linaweza kubadilishwa kuwa sehemu ya uzalishaji wenye tija.

Kwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, kuimarisha elimu ya kilimo cha mijini ni hatua inayoweza kuwasaidia wananchi kutumia fursa zilizopo, kuongeza uzalishaji wa mazao na kuimarisha kipato.

KUELEKEA DIRA 2050: KILIMO CHA MAARIFA, TEKNOLOJIA NA SOKO

Safari kuelekea Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 inahitaji sekta ya kilimo yenye tija, ubunifu na ushindani. Hii inamaanisha kuwa mkulima wa sasa anahitaji zaidi ya ardhi na nguvu kazi; anahitaji maarifa, teknolojia, taarifa sahihi na uelewa wa soko.

Pugu Kinyamwezi inatoa mfano wa namna elimu ya kilimo inaweza kuwafikia wananchi wa mijini na kuwasaidia kutumia fursa zilizopo kwa ufanisi zaidi.

Ujumbe kutoka kituoni hapo ni wazi: ardhi ndogo si kikwazo cha kuzalisha; maarifa, teknolojia na ubunifu vinaweza kuifanya kila nafasi kuwa fursa ya kilimo.

Kwa hiyo, Nanenane si maonesho ya mazao pekee, bali ni jukwaa la kujifunza, kubadilishana maarifa na kuona fursa mpya za kuongeza tija.

Na kupitia Pugu Kinyamwezi, kaulimbiu ya mwaka huu inapata maana ya vitendo: kutambua soko, kuongeza tija na kutumia sayansi, teknolojia na ubunifu kama msingi wa kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.



Jarida Hili Limetolewa Na;
KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
HALMASHAURI YA JIJI LA
DAR ES SALAAM

"Tambua Soko; Ongeza Tija Kutekeleza Dira 2050"